**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

**SHULE YA SEKONDARI GALANOS,**
**S. L. P. 5019,**
**TANGA.**

**Email: galanos5019highss@gmail.com**
**Website: www.galanos.sc.tz**
**Office No: 0736 646445**
**Headmaster: 0754 677126**
**secondMaster 0715332192**

***Kwa kujibu tafadhali rejea***

***Kumb. Na.*** GAL/T1/49/81 **June 2023**

---

Mwanafunzi: ______________________________

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (5) MWAKA 2023/2024 TAHASUSI CBA, PCM, HGE, HGK, ECA, EGM.**

1. Nafurahi kukuarifu rasmi kuwa umechaguliwa kuingia Kidato cha Tano (5) katika Shule hii.
2. Shule ipo ndani ya Jiji la Tanga kata ya Nguvumali kilomita 5 kutoka Tanga mjini na kilometa 4 toka Kange kituo kikuu cha mabasi. Hii ni Shule ya Bweni na ni ya Wavulana kwa kidato cha Tano na Sita.
3. Shule itafunguliwa tarehe13.08.2023**.** Kama hutofika mpaka tarehe ya **16.08.2023** nafasi yako itachukuliwa na kijana mwingine.
4. Usafiri; Toka kituo cha Mabasi ya mikoani Kange kuja shuleni:Bajaji shs 5,000/=, Tax 6,000/= Daladala 500/=,Bodaboda toka kituo cha dalala Majani mapana shs 1000/=.Chagua aina ya usafiri utakaona unakufaa kuweza kufika shuleni kwa gharama Ndogo.

**A: SHERIA ZA SHULE NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa *Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978na marekebisho yake kwa sheria na 10 ya mwaka 1995*. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:

1. Heshima na adabu kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa Walimu, Wafanyakazi wasio Walimu na Viranja.
3. Kuwahi kufika Shuleni na kutoondoka Shuleni kabla ya Shule kufungwa.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele).
6. Kuvaa sare ya Shule madarasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe,majumba ya starehe wala nyumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yeyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko.
11. Wizi, kuharibu mali/ kifaa cha Shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi na ni lazima alale kwenye kitanda na bweni alilopangiwa
13. Ni mwiko kutupa taka/ karatasi au uchafu ovyo ,au kuandika jambo lolote kwenye kuta za majengo
14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi Shuleni.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa Wafanyakazi bila ruhusa.
17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/ darasani au mahali popote ndani ya Shule.

18. **Ni marufuku** kwa mwanafunzi kuwa na **Simu** ya mkononi Shuleni, Adhabu kali itatolewa ikiwemo kulipia uharibifu wa Mfumo wa Umeme na Mzazi kumhamisha Mwanafunzi husika.Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
19. Kufeli au kutofanya Mtihani au kupata alama "F" kwenye Mitihaniwa somo lolote na mazoezi darasani ni kosa lisilo vumilika.
20. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
21. Ni marufuku mwanafunzi kubadili dini wala kumshauri mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**B: MIIKO MAALUMU:** **<u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.</u>**

a) Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya Kitaifa (sikukuu za Kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, maandamano, nk.)
b) Wizi (kuiba).
c) Kuoa au Kuolewa na kushiriki mahusiano ya jinsi moja.
d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
e) Kutohudhuria Shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa kwa zaidi ya siku tisini.
f) Kupigana au Kupiga mwanafunzi mwenzio au mwalimu au mfanyakazi yoyote .
g) Kuchochea ghasia/ kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama wa shule au watu,ikemo pia kugoma adhabu yoyote ile utakayowa na mwalimu.
h) Kuvuta sigara, kunywa pombe, bangi au dawa za kulevya ,kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
i) Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yoyote.
j) Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi, au mahakamani.
k) Kulala nje ya shule bila ruhusa
l) Kuwa na simu ya mkononi Shuleni au kifaa chochote cha simu.
m) Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kuua au kujiua kwa namna yoyote.
n) Ubakaji,Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.
o) Kutoka nje ya Shule nyakati za usiku.

**C: ULIPAJI WA MICHANGO YA MAENDELEO YA SHULE KWA KIDATO CHA TANO 2023.**

MCHANGANUO NA AKAUNTI NAMBA YA KULIPIA **NMB – BANK.**

| **Aina ya Michango** | **KIASI (JUMLA)** | **AKAUNTI NAMBA** |
|---|---|---|
| 1. Mchango wa Uendeshaji ..............................<br>2. Tahadhari ......................................................<br>3. Nembo ...........................................................<br>4. Kitambulisho cha Shule................................ | 65,000<br>5,000<br>5,000<br>5,000 | **Galanos Secondary School 41701200079** |
| **JUMLA MICHANGO YOTE** | **80,000/=** | |

**ZINGATIA: -Tafadhali fika na nakala halisi ya benki {BANK PAY IN SLIP (BPS).} yenye majina yako kamili yanayofanana na yaliyo kwenye nakala ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (Form Four Result Slip).**

- **Pia uje na rimu MBILI za karatasi nyeupe: (A4 Plain Paper-2)**
- **Uje na Stapler Machine aina ya Kangaroo.**
- **Uje na nakala (Photocopy) ya matokeo[Result slip] kwa ajili ya kuhakikiwa majina.**
- **Uje na nakala (Photocopy) ya Cheti cha kuzaliwa**
- **Hakikisha unaandika jina halisi la Mwanafunzi na Tahasusi (combination) yake wakati wakulipa fedha Bank kwenye Bank pay inslip.**

**SARE YA SHULE: MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**[A]: UTAPATA SHULENI SARE ZIFUATAZO :**

i. Suruali **mbili [2]** rangi nyeusi zenye mifuko miwili ya pembeni kwa mbele, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia, marinda mawili mawili kila upande kwa mbele. **Utashona shuleni kwa Fundi wa shule kwa shilingi 18,000/= kila moja.**

ii. Tai **mbili** nyeusi ndefu usawa wa tumbo isiyo na mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote (plain).Zinapatikana shule kwa shs 2,500/= kila moja.

iii. T-shirt **mbili maalumu rangi ya njano sare ya shule** zinapatikana shuleni kila moja shilingi 12,000 × 2 = 24,000/=

iv. Sare ya kushindia: S**uruali ya rangi ya kaki inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 18,000/=**

v. Picha (passport size) kwa ajili ya matumizi ya ofisi shilingi 3,000/=

**[B]: UJE NA SARE ZIFUATAZO:**

i. **Mwanafunzi aje akiwa amevalia tracksuit ya blue na t-shirt ya rangi ya bluu**,asije na nguo aina nyingine yoyote atakayekuja na nguo isiyo sare ya shule atarudishwa nayo nyumbani.

ii. Mashati mawili meupe (tetroni) ya mikono mifupi mfuko mmoja.

iii. Viatu vya ngozi vyeusi **vyenye kamba** jozi mbili, visiwe na visigino virefu. 'Safari boots na viatu vya wazi' haziruhusiwi.

iv. Soksi (stockings) jozi mbili au zaidi za rangi nyeupe, zinapatikana duka la shule.

v. Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana wa kawaida (usiwe na chater yoyote).

vi. Sweta si muhimu ila kama una ulazima njoo na sweta la rangi ya bluu lenye kola ya V.

vii. Mwanafunzi atokapo nje ya shule anatakiwa kuvaa **shati jeupe au T- Shirt ya Njano** ya shule na suruali nyeusi na anapaswa kuomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu.

viii. Nguo za michezo; mwanafunzi aje na: a). Tracksuit ya rangi ya Bluu,
b) Bukta ya rangi ya Bluu, c) T-Shirt ya rangi ya Bluu na d) Raba kwa ajili ya michezo.

**Uje na shilingi 5000/= kwa ajili ya uwekaji wa alama kwenye nguo na vifaa vyako binafsi ili kuepuka kuchukuliana na kuvaliana.

**USAFI BINAFSI WA MWILI:**

❖ Kufua nguo zako za Shule na Shuka kila wakati ni lazima.
❖ Nywele fupi za kuchana kwa kitana kidogo.
❖ Ndevu na mustachi havitakiwi.
❖ Kuoga kila siku ni lazima.
❖ Huruhusiwi kufuga kucha wala kupaka rangi ya kucha.
❖ Kuvaa kofia, bangili, hereni, kipini, kidani, (mkufu) na kikuku haviruhusiwi shuleni.
❖ Usafi wa chumba unacholala, chooni na eneo utakalo pangiwa ni lazima kila siku.

**UNUNUE VIFAA VIFUATAVYO KWA AJILI YA USAFI NA ELIMU YA KUJITEGEMEA**

| KIDATO CHA TANO HGK | KIDATO CHA TANO PCM,CBA,ECA,EGM,HGE |
|---|---|
| 1. Ndoo ya kudekia na mopa yake ______________ 12,000<br>2. Fagio la chelewa lenye mpini__3,000<br>3. Ndoo moja kubwa ya plastiki-- 7,000<br>4. Jembe na mpini wake______ 7,000<br>5. Slasher 1 5,000 | 1. Hard broom moja ______________ 3,500<br>2. Soft broom moja ___________________3,500<br>3. Drier/Squeezer moja _________________3,500<br>4. Ndoo moja kubwa ya plastiki __________7,000<br>5. Fagio la chelewa lenye mpini __________3,000<br>6. Brash ya kusafishia choo (Toilet brush) _3,000<br>7. Jembe na Mpini wake _______________ 7,000<br>8. Slasher 1 ----------------------------------- 5,000 |
| ***MUHIMU: Usisumbuke kubeba mizigo *vitu vyote vinapatikana duka la Shule** | |

i. Madaftari nane (8) (Counter book three (3) quires),na kalamu ya bluu/ nyeusi (Vinapatikana katika duka la shule)
ii. Mathematical set na Scientific Calculator.
iii. Sanduku la bati(Tranker) size ya kati. Masanduku mengine hayaruhusiwi.
iv. Karatasi za Rimu kwa ajili ya matumizi yako binafsi.
v. Begi la Darasani [School bag]

**ANGALIZO:**

Mwanafunzi aje na mahitaji yote kama ilivyo orodheshwa hapo juu .

**VIFAA VYA MALAZI NA CHAKULA VINAPATIKANA DUKA LA SHULE**

i. Godoro la **sponji jipya** lenye unene inchi 4 upana $2^1/_2$ na urefu wa futi 6. (shs 40,000) na Mto wa kulalia
**ii. Sahani, kikombe, kijiko na bakuli.(unaweza kununua duka la shule)**
iii. Chandarua ya duara ya rangi nyeupe.
iv. Shuka mbili sare ya shule zinapatikana shuleni kila moja Shilingi 8,000/=
* Blangeti na shuka za nyumbani haziruhusiwi*

**VIFAA/ MAHITAJI MENGINEYO:**

i. Fedha Za Mfukoni (Pocket money)

Ni muhimu kuwa na fedha za mfukoni ili uweze kujinunulia vifaa muhimu. Fedha hizo mwanafunzi atahifadhi mwenyewe. Mwanafunzi atalazimika kufungua akaunti benki, Shule inaweza kusaidia zoezi hilo la ufunguaji akaunti benki akifika shuleni.

****Ni lazima Umpatie shilingi 10,000/= kwa ajili ya kufungua akaunti ya Benki .Utatumia akaunti yako kwa ajili ya kuhifadhi fedha zako na wazazi kukutumia fedha ya Matumizi.**

**MAELEKEZO YA LIKIZO:**

Wakati wa likizo yoyote ile **NI LAZIMA** mwanafunzi aondoke/ arudi nyumbani. Hivyo basi, hakikisha unampatia/ umemtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani. Shule haiwajibiki kumpatia mwanafunzi nauli, chakula na malazi wakati wa likizo.

**HITIMISHO:**

i. Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa. Fomu hizo ni viambatanisho **A, B & C (Lazima zijazwe kabla ya mwanafunzi kufika Shuleni)**
ii. Shule hii ni ya Kilimo, Jiandae kujifunza kulima na kufuga kwa vitendo.
iii. Mwanafunzi aje akiwa amevaa Track Suit ya Rangi ya Bluu na T – Shirt ya Bluu.
iv. Mwanafunzi aripoti kabla ya saa kumi na mbili jioni.
v. Kufanya majaribio na mitihani na kuhudhuria maandalizi ya jioni [night preparation] ni **LAZIMA** sio hiari.
**vi.** ***Mwanafunzi akipatikana na Simu mzazi utalazimika pamoja na adhabu nyingine kulipia gharama za uharibifu wa miundombinu ya umeme na kumtafutia shule nyingine kijana wako [uwe tayari kumhamisha]***
**vii.** **Unapokuwa shuleni muda wote unapaswa kuzingatia utunzaji wa mazingira na miundo mbinu ya shule na matumizi bora ya vyoo,samani na vifaa mbalimbali vya shule na vya kwako binafsi.**
**viii.** **Unapaswa kuzingatia muda wa kukaa ndani ya eneo la shule, ukikamatwa nje ya Shule utapewa adhabu kali ikiwemo kuleta fence wire.**
**ix.** Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika Shule hii.
**x.** Kwa taarifa yoyote kuhusu kijana wako awapo shuleni na ili kuepuka utapeli wa kwenye mitandao ya simu. Pata ukweli wa taarifa kwa namba zifuatazo kabla ya kufanya chochote;

**A. MMKUU WA SHULE 0754 677 126**
**B. MAKAMU MKUU WA SHULE 0715 332 192**
**C. MWANDAMIZI MALEZI 0713 907 974**

***Ni matumaini yangu daima utatii sheria, taratibu na kanuni za Shule ili uje uvune kile kilichokuleta hapa – ELIMU.***

HONGERA NA KARIBU SANA

______________

SEMBE A. F

*KIAMBATANISHO "A"*

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALIMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

**SHULE YA SEKONDARI GALANOS**

**FOMU YA UTHIBITISHO NA MKATABA WA KUKUBALI KUJIUNGA NA GALANOS SHULE YA SEKONDARI**

***Makubaliano ya mkataba kati ya Mzazi,mwanafunzi na shule yatatekelezwa kama yalivyo kwa lengo la kufuta daraja sifuri na nne[ division 0 and iv]***

**[A]. IJAZWE NA MWANAFUNZI:**

*Picha ya Mwanafunzi*

1. Jina kamili la Mwanafunzi …………………………………………………………...
2. Uraia ……………………3.Dini…………………………………………………...
4. Tarehe ya kuzaliwa …………………Wilaya………………Mkoa…..…………....
5. Shule uliyohitimu kidato cha nne ……………………………………………..……..
6. Tahasusi (Combination) …………………………………………………….…….

Mimi ……………………………………………nikiwa na akili timamu na maarifa, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha …………… Naahidi kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Masharti mengine yote ya Shule,Ikiwemo kutopata alama F na 0 darasani, kutomiliki simu ya mkononi shuleni, utoro wa vipindi na kudharau baadhi ya masomo na mitihani..Endapo nitaingia kwenye makosa hayo mabaya naomba mzazi/mlezi wangu anitafutie shule nyingine na kunihamisha mara moja. Nakubaliana na hoja zilizoanishwa hapo juu na kwenye fomu ya kujiunga na shule ya Sekondari Galanos na kuzizingatia na kuzifuata.

Jina la mwanafunzi………………………………… Sahihi ya Mwanafunzi …………………… Tarehe ya mkataba …………………………………

**[B]. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI ATAKAYETAMBULIWA NA SHULE**

*Picha ya Mzazi/ Mlezi*

1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi ………………………………………………….….
2. Anuani kamili ……………………………………………………………..…....
3. Kazi unayofanya ……………………………………………………………….
4. Namba ya simu: [a]Nyumbani …………………………………………………
   [b]. Ofisini ……………………[c] Mkononi……………………………
   .[d]. Wilaya ………………………. [e] Mkoa ……………………………..…

Mimi ……………………………….………… Mzazi/ Mlezi wa ………………………………..…

Nikiwa na akili timamu ,nimesoma vyema Sheria, Taratibu na Kanuni za Shule, Nakubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Galanos. Endapo Mwanangu ataenenda kinyume na Sheria/ taratibu za Shule na kupatikana na kosa la kupata alama F na 0, kumiliki simu ya mkononi shuleni, na kushiriki utoro wa vipindi, kukwepa mitihani na kudharau baadhi ya masomo, kama ilivyoainishwa hapo juu nakubali nikabidhiwe kijana wangu ili nimtafutie shule nyingine ili kuepusha madhara na majanga kwa wanafunzi wengine na niweze kumsimamia kwa karibu na sitakuwa na pingamizi ya aina yoyote juu ya jambo hili kwani nafahamu fika kwamba kilichomleta shule ni kusoma na si vinginevyo.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi ……………………………………. Tarehe ……………………………

**C. UTHIBITISHO WA SERIKALI ZA MITAA**

Jina la M/Kiti wa Mtaa au M/Mtendaji wa Kijiji………………………………………

Sahihi ………………………Namba ya Simu…………………………..Muhuri…………………

**MKUU WA SHULE**

***KIAMBATANISHO "B"***

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**GALANOS SECONDARY SCHOOL**

***STUDENT MEDICAL CERTIFICATE***

(To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Galanos Secondary School P. O. Box 5019, TANGA)

To the Medical Officer,

………………………………………….
………………………………………….
………………………………………….

**RE: ______________________________________________________**

Please, examine the Student mentioned above and comment in his health by responding to the following items. Kindly put a Tick (v) or Cross (x) in front of either YES or NO as you find appropriate.

*SEMBE .A.F*

**HEADMASTER GALANOS SECONDARY SCHOOL**

Does a student have problems in connection with?

a) Sight? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

b) Hearing? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

c) Speech? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

d) T. B (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

e) Blood pressure? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

f) Any Physical disability? (1) No (2) Yes
If yes, state ………………………………………………………………………………

Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this School?
(1) No (2) Yes. If no, please state reasons.

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

*Date ……………………………. Name and Signature of M. O ………………………………………......*

*Designation and stamp …………………………………………………….*

*KIAMBATANISHO "C"*

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALIMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

SHULE YA SEKONDARI GALANOS

---

## FOMU MAALUMU YA UTAMBULISHO
## IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI

### A: TAARIFA YA MZAZI AU MLEZI:

**(i) NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA)**

| | |
|---|---|
| BABA | |
| MAMA | |
| MLEZI | |

**JINA KAMILI**

| JINA LA KWANZA | JINA LA KATI | JINA LA MWISHO |
|---|---|---|
| | | |

**JINSIA**

| ME | KE |
|---|---|
| | |

**(ii) MAHUSIANO NA MZAZI/MLEZI**

| |
|---|
| |

**BARUA PEPE**

| |
|---|
| |

**NAMBA YA SIMU**

| | |
|---|---|
| KAWAIDA | |
| WHATSAP | |

| (iii) KAZI YAKO | ANUANI YAKO | ANUANI YA MAKAZI | KIWANGO CHA ELIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |

### B: TAARIFA ZA MWANAFUNZI:

| (i) JINA LA KWANZA | JINA LA BABA | JINA LA UKOO | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| | | | |

**(ii) TAREHE YA KUZALIWA**

| SIKU | MWEZI | MWAKA |
|---|---|---|
| | | |

**JINSIA**

| ME |
|---|
| |

**NAMBA YA CHETI CHA KUZALIWA**

| |
|---|
| |

**(ii) HALI YA WAZAZI**

| BABA | |
|---|---|
| **HAI** | **AMEFARIKI** |

| MAMA | |
|---|---|
| **HAI** | **AMEFARIKI** |

| MZAZI MMOJA | |
|---|---|
| **BABA** | **MAMA** |

| WAZAZI WAWILI |
|---|
| |

SEMBE A. F

**MKUU WA SHULE**